wa Kata
Tarafa ya
mkoani
kichota
moja ya
yojengwa
li wa
a Hifadhi
goro

HABARILEO UK 9.

# Wafugaji wanavyofaidi huduma za maji Hifadhi ya Ngorongoro

**Na Mwandishi Wetu**

"UHUSIANO uliopo kati ya jamii ya wafugaji na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) unachangiwa na huduma mbalimbali za kijamii zinazotolewa na Mamlaka kwenda kwa jamii maana kama huduma hizi zitakuwa mbaya, basi hata uhusiano hautakuwa mzuri. Ndiyo maana bajeti zetu zinazingatia pia mahitaji halisi ya jamii inayoishi ndani ya hifadhi."

Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi anayesimamia Idara ya Maendeleo ya Jamii katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Mdala Fedes, anasema hayo anapoelezea namna hifadhi hiyo inavyonufaisha jamii ya wafugaji wa Kimasai hususan wanaoishi katika Tarafa ya Ngorongoro wilayani Ngorongoro katika Mkoa wa Arusha hasa maji kwa matumizi ya watu na mifugo.

Uchunguzi kupitia mazungumzo na vyanzo mbalimbali katika Hifadhi ya Ngorongoro umebaini kuwa, katika eneo la hifadhi baadhi ya shughuli za kibinadamu kama kilimo na ujenzi wa nyumba za kudumu haziruhusiwi, hivyo Hifadhi imekuwa ikiwasaidia wakazi wa eneo hilo kwa namna mbalimbali kwa kuwa uchumi wao unategemea mifugo zaidi.

Anapotakiwa kufafanua namna NCAA inavyowasaidia na kuwanufaisha wanajamii hao kupitia ufugaji, Fedes anasema: "Kupitia wataalamu wetu wa NCAA, tunatibu wanyamapori na mifugo ya wafugaji hawa ndiyo maana mifugo yao yaani ng'ombe, punda, mbuzi na kondoo wakipata magonjwa, wanatoa taarifa kwetu na tunaitikia haraka kwa matibabu na chanjo yaani kinga."

Fedes anasema kutokana na wanajamii hao kuzuiwa kufanya shughuli za uzalishaji mali, Mamlaka inatoa na kuwapa baadhi ya huduma kwa kuwa nao ni sehemu ya hifadhi na wanasaidia katika uhifadhi kwa kuwa wametawanyika eneo lote la hifadhi hivyo, kuwa vigumu hata kwa majangili kupenya.

Anasema: "Bahati nzuri, Wamasai wenyewe hawana asili ya kula nyama ya wanyamapori hivyo hawawindi wanyamapori, kwa maana hiyo wanasaidia sana uhifadhi na pia kuvutia utalii katika hifadhi kutokana na umaarufu wa kabila lao unaovutia watalii wengi wanaotembelea Ngorongoro."

Anasema idara yake imekuwa ikigharimia miradi mbalimbali ikiwemo ya uboreshaji wa mifugo, chanjo na maji kwa ajili ya matumizi ya watu na

Inaendelea Uk. 13

Scanned with CamScanner

viongozi kadhaa wasio na ulemavu

Mmoja alinukuliwa wakati wa tathmini hiyo akisema: "Kiongozi mmoja wa chama cha siasa alinizuia kujiandikisha eti kwa kuwa ni mlemavu."

### CHANGAMOTO ZA WANAWAKE

Ilibainika katika tathmini hiyo kuwa, bado jamii inao mfumo dume unaopotosha na kuwafanya baadhi ya watu kudhani kimakosa kuwa, wanawake hawawezi kuongoza.

Uchunguzi unaonesha kuwa, wanawake ni wachapa kazi wazuri na waadilifu wanapokuwa madarakani. Mfano wa wanawake viongozi wanaofanya vizuri, ni pamoja na Makamu wa Rais, Samia Suluhu ameonesha uwezo mkubwa katika wadhifa wake.

Ripoti inasema: "Vyama vingi havizingatii kwa usawa, suala la jinsia kutokana na kutawaliwa na mfumo dume dhidi ya wanawake."

Inaongeza: "Wanawake wengi walilalamika kukosa nguvu za kiuchumi ili kupambana na washindani wao wanaume wanaotumia mwanya huyo kujipatia wapiga kura."

Changamoto nyingine inayotajwa na ripoti ya tathmini hiyo ni muda wa mambo ya siasa hasa uchaguzi, kugongana na ratiba ya majukumu ya kifamilia.

"Wanawake wengi waliohojiwa walisema walishindwa kushiriki kikamilifu katika uchaguzi kutokana na ratiba ya mikutano ya kampeni ambazo mara nyingi ni jioni muda ambao wanapaswa kuwa nyumbani wakiandaa chakula cha jioni..." anasema Zaa.

### MAPENDEKEZO YA JUMLA

Inapendekezwa kuwa, ili kuwapo ushiriki kamilifu wa wanawake na watu wenye ulemavu katika siasa na mchakato wa uchaguzi, kufanyike marejeoya sheria ili kuhakikisha kunakuwapo demokrasia shirikishi katika vyama vyote kwa wanawake na watu wenye ulamavu.

"Serikali na vyama vya siasa viwasaidiwe wanawake na watu wenye ulemavu wanaotamani kugombea ili kuwawezesha kukamilisha ushindani na washindani wao wanaume," anasema Zaa na kuongeza: "Asasi za kiraia zinazojihusisha na jinsia na ushirikishwaji jamii kufanya kazi kwa karibu na vyama vya siasa katika kuelimisha viongozi wa vyama na makada kuhusu jinsia na ushiriki wa wanawake na watu wenye ulemavu katika mchakato wa demokrasia na uchaguzi."

# Wafugaji wanavyofaidi huduma za maji Hifadhi ya Ngorongoro

Inatoka Uk. 9

mifugo.

"Kwa asili ya Wamasai, ni wafugaji na nguvu yao kubwa inategemea ufugaji hivyo, tunawasaidia na kuwawezesha katika eneo hili la ufugaji ili wapate mifugo bora yenye afya ya kutosha ili iwasaidie kupata kipato kizuri huku ufugaji wao ukiwa endelevu na tunafanya hivi hasa kupitia huduma za chanjo dhidi ya magonjwa ya mlipuko kwa wanyama."

"Hili tunalifanya ili kuepusha magonjwa kutoka kwa wanyamapori kwenda kwa mifugo; au magonjwa ya mifugo kwenda kwa wanyamapori. Kwa mfano, ng'ombe akifa porini kama alikuwa na ugonjwa, ataacha vijidudu na mnyamapori akila nyasi zilizoota pale, anaweza kupata vijidudu hivyo vinavyoweza kudhuru afya yake, ndiyo maana tunanunua pia dawa za chanjo kutibu mifugo wao," anasema Fedes.

Hivi karibuni Kamishina huyo Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi alinukuliwa akisema: "... Tunafanya pia uhamilishaji ili kuboresha mifugo wao maana wengi wanakuwa dhaifu na kushindwa kushindana katika soko ili kupata bei za soko shindani hivyo, tunawatafutia mbegu bora na kupandikiza ili ng'ombe wawe bora zaidi."

Anapoulizwa kuhusu upigaji chapa kama alama ya mifugo, lakini kwa kuzingatia ulinzi wa thamani ya ngozi, Fedes anasema: "Idara hii kwa kushirikiana na Halmashauri ya Ngorongoro, tulitengeneza mihuri mbalimbali na kila kijiji kikapata namba yake ili kujua mwingiliano uliopo."

Anasisitiza: "Uwekaji wa chapa (alama) hizi unafanyika kwenye miguu chini ya goti la ng'ombe na siyo juu ili kutoharibu ngozi na thamani yake..."

Kwa mujibu wa sensa iliyofanyika mwaka 2017 ndani ya hifadhi hiyo, eneo hilo lina mifugo takriban 831,500.

Mintarafu suala la maji kwa mifugo na binadamu, Fedes anasema: "Tunachangia utoaji wa huduma za maji kwa ajili ya mifugo na binadamu ndiyo maana tumechimba mabwawa mengi na majosho kwa ajili yao."

"Huwa tunafanya utafiti na kuangalia eneo lenye ukingo na kutengeneza ili kuvuna maji yanayotuama mwaka mzima na kuyapeleka sehemu za kunyweshea ili kuzuia ng'ombe kunywa kwenye bwawa."

Uchunguzi umebaini kuwa, katika kuwanufaisha wanajamii kiufugaji, NCAA imewezesha eneo hilo kuwa na mabwawa 21 na majosho 17 kwa ajili ya mifugo.

Kuhusu maji kwa matumizi ya watu, Fedes anasema: "Tumeweka maji ya bomba katika vijiji vingi ndani ya hifadhi... Katika vijiji vingine vipo visima virefu na pampu ya jenereta ya mafuta na sehemu nyingine, tumeweka pampu za kutumia umeme unaotokana na mionzi ya jua (sola)."

Licha ya kuwepo kwa miradi kadhaa ya maji inayosimamiwa na NCAA, imebainika kuwa Mamlaka hiyo inaendesha visima vinne vya Oldonyoogol na Lemuta (kinachotumia jenereta) vinavyonufaisha wakazi wa maeneo ya Kesile, Esilalei, Elerai na Oldonyoogol huku Kisima cha Kakesio kinachotumia jenereta kikinufaisha wakazi wa Kakesio, Ereko na Ngutot.



Meneja wa Maendeleo ya Jamii wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Fedes Mdala (aliyesimama) akizungumza katika mkutano wa kujadili utaratibu wa usimamizi wa fedha zinazotolewa na NCAA kwa Baraza la Wafugaji na miradi inayotekelezwa katika Tarafa ya Ngorongoro (Picha kutoka Mtandaoni).

Kisima cha Osinoni kinahudumia pia wakazi wa maeneo ya Osinoni, Ngereyani na Loorkisale. Chanzo cha maji cha Mto Orpusare kinanufaisha wakazi wa maeneo ya Olpiro, Endumaghay na Endamagha.

"Karibu vijiji vyote vina huduma ya maji kupitia mifereji inayopeleka maji katika vijiji vingine," anasema Fedes na kuongeza: "Kisima cha Oldonyoogol kinachotumia sola huzalisha lita 800,000 kila siku na ni kizuri kwa ufugaji wa kondoo ndiyo maana hata wafugaji wengine wa kata takriban 11 zikiwamo za kutoka nje ya Hifadhi ya Ngorongoro, wakati mwingine hutumia kisima hicho."

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Maji NCAA, Victor Joseph Gwandu anasema changamoto kubwa katika miradi ya maji inayotekelezwa na NCAA kwa wakazi wa eneo la hifadhi, ni baadhi ya wafugaji hao kuiharibu ili kupata maji ya kunyweshea mifugo wao katika sehemu wanazotaka wao.

"Changamoto nyingine ni uhamaji wa wafugaji kwenda baadhi ya maeneo yasiyo rafiki kwa miradi ya maji kama milimani na pia, idadi kubwa ya mifugo kutoka maeneo ya nje ya tarafa hii," anasema Victor na kuongeza kuwa, wanapambana na hali hiyo kwa kuendelea kuwapa elimu endelevu juu ya umuhimu wa kutunza miradi hiyo ambayo Serikali imekuwa ikitoa fedha nyingi kuijenga.

Fedes yeye anasema: "Changamoto kubwa ni wafugaji kuhamahama na pia, baadhi ya wananchi wamejenga kasumba ya utegemezi klasi kwamba, hata bomba likiharibika sehemu ya kutengeneza kwa Sh 10,000 mtu anaweza kulalamika na kusubiri mamlaka itengeneze."

"Ili kukabiliana na hali hiyo, tumepanga kuwasaidia na tumewashauri waunde umoja wa watumiaji maji ili kusaidia kutunza na kulinda vyanzo na miundombinu ya maji..." anasema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Malisho katika Baraza la Wafugaji wa Tarafa ya Ngorongoro ambaye pia ni Kiongozi wa Mila (Laigwanani) mkazi wa Kijiji cha Kayapsi, Saimon Saitoti anakiri akisema: "Ni kweli awali kulikuwa pia na uchimbaji holela wa visima unaoharibu mazingira na hata wakati mwingine wanyama kufa kwa kudumbukia katika visima hivyo, lakini tunaendelea kuhamasishana kuacha kabisa suala hili..."

Anaongeza: "Tumejengewa sehemu ya kunyweshea mifugo, ingawa iko mbali na wakati mwingine, maji yanakatika inakuwa shida..."

Mmoja wa wanawake katika Kitongoji cha Elmotonyi katika Kata ya Ngorongoro, Nasaro Samlia anasema: "Kwa kweli tunashukuru hifadhi maana tuliwekewa bomba la maji japo kwetu lipo mbali na watu ni wengi, hivyo wakati mwingine tunakosa. Hata hivyo, ni msaada mkubwa kwetu..."

Mwingine anayekataa kutajwa anasema: "Walio nje wanaweza wasijue namna hifadhi inavyotusaidia, lakini inatumia pesa nyingi kwa ajili yetu wakazi wa humu; mamilioni kwa mamilioni. Kwa kweli tunaishukuru Serikali maana hifadhi ni mali ya serikali."

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kayapsi katika Kata ya Ngorongoro, Osoyi Naitwati anasema: "Hapa tumepata josho na kama kijiji linatusaidia sana maana tayari tunayo hata akaunti, ingawa josho lipo mbali kwa baadhi ya wafugaji kwa kuwa baadhi huwa wanasogea pembezoni kwa ajili ya kufuata malisho."



Moja ya mabwawa ya maji kwa ajili ya kunyweshea mifugo ya wenyeji lililojengwa eneo la Simba B ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Scanned with CamScanner

Jumatatu 15 Juni 2020
www.timesmajira.co.tz



# Ufugaji ng'ombe inavyowezesha kuzalisha nishati

*Na Mwandishi Wetu*

UFUGAJI ni miongoni mwa sekta chache ambazo imekuwa zina mchango mkubwa nchini kwa kukuza pato la taifa na mfugajibinafsi.

Hadi mwaka jana, 2019, sekta hiyo ilikuwa kwa asilimia 5 na kuchangia asilimia 7.4 kwa pato la taifa.

Kwa kutambua mchango wa sekta ya ufugaji nchini, serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, iliamua kuwekeza kwenye mashamba ya mifugo ili kuyawezesha yazalishe mifugobora, itakayosaidia kukuza kipato cha taifa na wananchi wanaojihusisha na shughuli zake pamoja na ujasiriamali unaotokana na mazao yake.

Moja ya mashamba ambayo serikali imewekeza ni Shamba la Mifugo Sao Hill lililopo Kata ya Ikongosi, Kijiji cha Ifulavanu Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa.

Akizungumzia historia ya shamba hilo, kaimu meneja Mtama Galusi anasema kuwa, Shamba la Mifugo Sao Hill lilianzishwa mwaka 1967 baada ya serikali kulitaifisha kutoka kwa wakulima wa Kizungu.

Anasema kuwa mwaka 1968 shamba hilo lilianza kufanya kazi rasmi kwa kutumika kama shamba la kuzalisha mitambabora, ili iuzwe kwa wafugajiwadogo katika maeneo ya Nyanda za Juu Kusini nchini.

Galusi anasema kuwa, shamba hilo imekuwa linazalisha vizuri, sababu ya hali ya hewa nzuri ya baridi, inayosaidia wanyama wanaofugwa wanawiri vizuri, tofauti na mashamba mengine ambayo yapo ukanda wa joto.

Anasema kuwa, kwenye shamba hilo pia kuna maji ya Mto Ruaha, ambayo hutiririkia kwenye Bwawa la Mtera, hivyo kwamba hutumika kunywesha mifugo kiasi cha kutosha tofauti na mashamba mengine.

Akizungumzia kuhusu mafanikio ya shamba hilo tangu kuanzishwa kwake, Galusi anasema kuwa kuna ng'ombe 1,600, hivyo kwamba limetumika kuzalisha mitamba mingi, inayouzwa bei nafuu kwa wafugajiwadogo katika mikoa ya Iringa na Mbeya pamoja na wilaya zake.

"Katika Wilaya ya Rungwe na Halmashauri ya Wilaya ya Mji wa Busokelo mkoani Mbeya, kuna ng'ombe wengi wa maziwa ambao zao lake linatokana na Shamba la Sao Hill," anasema.

"Wilaya hizo zilifaidika na utaratibu waliouanzisha wa 'Kopa Ng'ombe Lipa Ng'ombe', utaratibu ambao uliwanufaisha wananchi wengi."

Aidha, anasema kuwa shamba hilo limeweza kuzalisha malisho, ikiwa ni pamoja na mbegu za malisho wanazouziwa kwa bei nafuu wafugaji wadogo wa mikoa ya Iringa na Mbeya.

"Mbali na hiyo, ndani ya shamba hilo lina fursa ya kuuza ng'ombe wake kwa bei nafuu," anasema huku akitaja mfano kwamba, bei ya mtamba mwenye mimba ni sh. 1,600,000, tofauti na mashamba ya watubinafsi yaliyopo Wilaya ya Mufindi, ambayo bei zake inafika sh. 3,000,000 hadi 4,500,000.

"Serikali imekuwa ikiwajali na kuwapa wafugaji mitambabora kwa bei ambayo kila mtu anaweza kununua, ila miongoni mwa changamoto zinazowakumba ni pamoja na uchache wa vitendeakazi, hususani usafiri wa kutembelea maeneo ambayo yana mifugo.

"Kuna baadhi ya maeneo ambayo yapo umbali wa kilomita sio chini ya 10, hivyo bila usafiri inakuwa shida kufika katika eneo husika.

"Changamoto nyingine ni kuwa, eneo hilo lina mvua nyingi zinazosababisha kupungua kwa madinijoto, ambayo ni muhimu kwa mifugo, jambo ambalo linawalazimu kununua madini hayo kwa bei kubwa," anasema.

Kuhusu matarajio yao kwa shamaba hilo, Galusi anasema kuwa, hadi kufikia Juni mwaka huu 2020 wanatarajia iwe wamesambaza mitamba aina ya Borani kati ya 120 hadi 130, sababu uhitaji wa ng'ombe hao bado ni mkubwa.

Kwamba mitambadume hao aina ya Borani husaidia kuboresha kosaafu za ng'ombe wa asili wanaofugwa zaidi na wafugajiwadogo.

Mkurugenzi idara ya malisho shamba hilo Dkt Asimwe Rwiguza, anasema kuwa wafugaji wengi bado wanategemea malisho ya asili, ambayo kimsingi hayatoshelezi na hayana viinilishe vya kutosha, hivyo wamehimiza wafugaji waandae mashamba ya malisho na kutumia mbegubora zinazopatikana kwenye mashamba ya serikali, ili waweze kuboresha lishe za mifugo yao.

Anasema kuwa, wizara kupitia idara ya malisho na uendelezaji rasilimalimifugo, imeendelea kusambaza uelewa kwa wafugaji kuhusu uzalishaji na utunzaji wa malisho.

Akizungumzia faida ya ziada anayoweza kuipata mfugaji wa ng'ombe, anasema kuwa, ufugaji ng'ombe pia inaweza kuwa na faida zaidi, kama wafugaji wataendelea kuelimishwa kiasi cha kutosha hadi kuweza kutambua faida nyingine, zaidi ya kuvuna nyama, maziwa na ngozi tu.

"Faida ya ziada anayoweza kuipata mfugaji kutoka kwa ng'ombe aliyefugwa ni pamoja na nishati ya gesi, ambayo kitaalamu inaitwa 'biogas'.

"Nishati hii ya gesi inaweza kupatikana kutokana na kinyesi cha ng'ombe, ambacho wengi wanakiita samadi.

"Wafugaji wakielimishwa na kuhamasishwa vizuri kutumia njia hii m'badala ya matumizi ya nishati ya gesi inayotokana na samadi, na faida zake, huenda itasaidia kupunguza matumizi ya kuni, ambayo kwa muda mrefu sasa serikali imekuwa ikiyapiga vita, kwani yanatajwa kuwa ni chanzo kikubwa cha uharibifu wa mazingira na uoto wa asili nchini," anasema.

Naye mkulima katika Kijiji cha Igowole,Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa, Michael Mhosole ambaye pia ni mfugaji, anayefuga ng'ombe wa kisasa, anasema kuwa, pamoja na faida ya maziwa anayopata kutokana na ufugaji wa ng'ombe hao, pia hupata nishati ya gesi, ambayo huitumia kwa matumizi ya nyumbani kwake.

Anasema kuwa, anapata nishati hiyo ya gesi baada ya kujenga mtambo unaotumika kuchakata samadi ya ng'ombe na kuibadilisha kuwa nishati ya gesi, ambayo huitumia kwa ajili ya kupikia. Mhosole anasema kuwa nishati ya gesi inayotokana na ng'ombe, ikitumika vizuri, husaidia kupunguza matumizi ya kuni na mkaa.

"Serikali na wataalamu wakiwajengea wananchi uwezo na elimu ya kutosha kuhusu matumizi ya nishati ya gesi inayotokana na samadi, itakuwa ni chanzo kizuri cha ajira kwa vijana.

"Baada ya samadi hiyo kutumika kama chanzo cha nishati, hutolewa na kupelekwa shambani na kwenda kutumika tena kama mbolea ya kukuzia mazao," amesema.



Michael Msohole akionyesha mtambo wake wa kuzalisha gesi kwa kutumia kinyesi cha ng'ombe, ambayo huzalisha nishati ya umeme. (Na Mpigapicha Wetu)

Scanned with CamScanner